

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 1

## 28 Watu wa Mungu wanavuka Mto Yordani

**Kwa Biblia** Yoshua mlango wa 3 na mlango wa 4: 1-7

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu alisaidia watu wake kuingia kwa Nchi aliyowaahadi.

### Somo

Yoshua na watu wote walifurahi waliposikia habari iliyoletwa na wapelelezi kuhusu Yeriko. Wapelelezi walisema kwamba watu wa Yeriko walikuwa dhaifu na waoga kwa sababu walijua Mungu alikuwa anawasaidia Waisraeli. Waisraeli walipata nguvu. Walikuwa tayari kwenda kupiga na kuchukuwa Kanaani.

Waisraeli walikuwa na shida. Walipiga kambi kwa mpaka wa nchi ya Kanaani. Mto wa Yeriko ulikuwa katikati yao na nchi hiyo. Waisraeli walitakiwa wavuke Mto wa Yordani ili waingie kwa nchi ya Kanaani.

Kingo za Mto wa Yordani zilikuwa zimefurika. Mafuriko yalikuwa yanachukuwa karibu miezi miwili. Waisraeli walikuwa karibu milioni mbili na walikuwa na mbuzi na kondoo wengi. Hawa watu wote na mifugo wangevuka namna gani huo mto uliofurika.

Yoshua aliangalia n'gambo ya mto na kuona Nchi ya ahadi. Labda alikumbuka miaka arobaini iliyopita wakati Waisraeli walikuwa kando ya Mto wa Shamu. Mungu aliwasaidia Waisraeli kuvuka Mto wa Shamu. Yoshua aliamini kwamba Mungu atawasaidia tena.

### Maswali

1. Nini ilizuia Waisraeli kwenda kwa nchi ya Kanaani?
2. Yoshua aliuliza nani asaidie?
3. Mungu alipea Waisraeli nini kuwaongoza jangwani?
4. Mungu aliondoa nguzo ya wingu na moto lini?
5. Waisraeli walitakiwa kuwa na nini kuonyesha kwamba Mungu alikuwa bado nao?
6. Makuhani walifanya nini?
7. Nini ilifanyika makuhani walipokanya ndani ya Mto wa Yordani?
8. Yoshua na Waisraeli walitii maagizo ya Mungu sawasawa?
9. Watu 12 walifanya nini?
10. Waisraeli walifanya nini walipofika kwa nchi yao salama?

### Majibu


1. Mto wa Yordani ulikuwa umefurika kwa hivyo Waisraeli hawangeweza kuvuka.
2. Yoshua aliuliza Mungu awasaidie.
3. Nguzo ya wingu na nguzo ya moto iliongoza Waisraeli.
4. Mungu aliondoa hizo wingu walipofika nchi ya Kanaani.
5. Waisraeli walikuwa na Sanduku katika Maskani.
6. Makuhani walibeba Sanduku mbele ya Waisraeli.
7. Mto wa Yordani uliacha kwenda. Kulikuwa na njia kavu ya Waisraeli kutumia kuvuka mto.
8. Ndiyo. Walitii Mungu sawasawa.
9. Watu 12 walichukuwa mawe 12 kutoka katikati ya mto. Walijenga tuta kubwa ya mawe upande mwингine wa mto kuwakumbusha muujiza wenye Mungu alifanya kuwasaidia wavuke.
10. Waisraeli walifanya karamu ya Pasaka, kusifu na kushukuru Mungu.

Yoshua aliomba Mungu. Mungu alikuwa amesaidia Musa. Mungu aliahidi kusaidia Yoshua pia. Mapema asubuhi yake, Yoshua aliita watu wote kando ya kingo za Mto wa Yordani. Mungu alielezea Yoshua vile watavuka Mto.

Yoshua alipea viongozi wa Waisraeli amri. Lazima watu watii Mungu sawasawa. Halafu atawasaidia wavuke Mto wa Yordani.


Mungu alikuwa amewaongoza Waisraeli jangwani. Mungu aliwapa nguzo ya wingu mchana na nguzo ya moto usiku. Hii iliongoza Waisraeli, tena ilionyesha kwamba Mungu ako nao. Safari ya Waisraeli ilikwisha walipofika Mto wa Yordani. Mungu aliondoa nguzo ya wingu na nguzo ya moto. Lakini Mungu alikuwa bado nao.

Maskani yenyé Musa alitengeneza kulikuwa na pahali Patakatifu Sana. Ndani yake kulikuwa na Sanduku. Hilo Sanduku lilifunika na mabawa ya dhahabu ya makerubi na hapo ndipo Mungu aliiishi. Mungu aliondoa nguzo ya wingu na nguzo ya moto. Lakini Waisraeli walibaki na Sanduku ndani ya Maskani. Kwa hivyo Mungu alikuwa bado ako nao.



Mungu aliambia Yoshua jinzi ya kuvuka Mto Yordani. Makuhani walibeba Sanduku mbele ya kila mtu. Makuhani walibeba Sanduku mpaka kando ya Mto. Waisraeli walifuata kwa hatua nyuma ya Sanduku. Walitazama vile makuhani walifika kando ya maji.

Makuhani waliendelea kwenda hata walipofika kando ya maji. Waliendelea pole pole. Waisraeli wote walitembea nyuma yao. Makuhani walipo kanyaga ndani ya maji, mto uliacha kwenda. Maji yalifanya mlima mrefu. Mungu alitengeneza njia kavu kwa mto. Waisraeli walitembea katikati ya mto kwa njia kavu.



Makuhani walipofika katikati ya mto, walismama. Makuhani walismama na Sanduku kwa njia kavu katikati ya mto. Waisraeli wote walivuka Mto wa Yordani kwa njia kavu.

Mungu aliambia Yoshua achague mtu mmoja kutoka kwa kila kabilia ya Israeli. Wale watu kumi na wawili walienda katikati ya mto. Kila mmoja aliokota jiwe kubwa, nyororo kutoka chini kabisa ya mto. Walibeba hayo mawe kumi na mbili mpaka upande mwengine wa Mto wa Yordani. Yoshua alipanga tuta ya hayo mawe kumi na mbili. Mawe yalikuwa ya kukumbusha Waisraeli muujiza mkubwa uliofanya na Mungu kuwasaidia wavuke Mto wa Yordani. Siku sijazo, watu wataauliza, "Haya mawe yana maana gani?" Waisraeli watajibu, "Mungu alikausha maji ya Mto wa Yordani hapa. Waisraeli walivuka mto kwa njia kavu." Hapo watu watakumbuka kwamba Mungu ni wa nguvu. Watampenda na kumtii.

Waisraeli walivuka Mto wa Yordani salama. Wote walivuka mto na kuingia nchi yenyé Mungu alikuwa amewaahidi. Watu wote walipokuwa wamevuka, makuhani walibeba Sanduku kutoka katikati ya mto na kuenda mpaka upande mwengine. Bunde tu makuhani walipotoka nje ya mto, maji ya mto yalirudi tena. Mto wa Yordani ulifurika tena.

Mungu alileta Waisraeli kwa nchi yao yenyé alikuwa amewaahidi. Furaha gani ilikuweko siku hiyo! Yoshua na Waisraeli walifanya karamu ya Pasaka. Walishukuru na kumsifu Mungu kwa kuwahurumia na kuwapenda.